OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
SHULE YA SEKONDARI KIWELE

S.L.P 733
IRINGA
Barua pepe…
Mob: 0767 884095/0713 280696
Tarehe 30/11/2020

Kumb Na KWSS/AD/VOL.1/16
JINA LA MWANAFUNZI……..
S.L.P……
IRINGA

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIWELE WILAYA YA IRINGA (V) MKOA WA IRINGA KIDATO CHA KWANZA- 2021.**

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari kiwele ipo umbali wa kilomita ishirini na tano (25) magharibi mwa mkoa wa Iringa/ halmashauri ya wilaya ya Iringa.

Usafiri wa basi kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi yanayofanya safari za **M.R - Kitapilimwa** kilichopo karibu na **M.R HOTEL ua stand kuu - Itagutwa** nauli ni **Tsh 2,000/=**

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 17/01/2021 ndani ya siku saba.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za shule

a) Sare ya shule hii ni suluali za kaki 2 zisizo pungua kipenyo cha sentimita 15 miguuni na shati nyeupe 2 za mikono mifupi kwa wavulana na sketi za kaki 2 na shati 2 nyeupe mikono mifupi . Kwa wasichana sketi zinashonwa za

malinda madogo ya kawaida. kitambaa ni kizito ambacho mfano wake umeambatanishwa na fomu hii.

- Viatu vyeusi vya kamba jozi mbili (02) vinavyopigwa rangi.
- Soksi nyeusi jozi mbili (02) kwa wavulana na soksi ndefu nyeupe kwa wasichana.
- Sweta rangi ya bluu, shingo ya 'V'

NB: - Nywele ni sehemu ya sare ya shule, zinatakiwa ziwe fupi za kuchana, aidha kucha ziwe fupi na safi wakati wote. Hairuhusiwi kuvaa mapambo ya aina yoyote ile shuleni vilevile mwanafunzi haruhusiwi kufuga ndevu.

b) Rangi ya hijab ifanane na sare ya shule.

c) Sare ya michezo kwa shule hii ni tshirt ya rangi za njano (kampuni ADIDAS) isiyo na maandishi ya aina yoyote. 2 na track suit za kijani (yenye mistari myeupe ubavuni) 2 pamoja na raba nyeupe kwa wavulana na wasichana.

2.2 Daftari (counter book quire 3) 12, kalamu 12 na mkebe wa hesabu – 01, rula -01. Mzazi /mlezi utatakiwa kumpa mwanao nauli ya kuja shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu.

2.4 Pia mzazi/mlezi wa mwanafunzi wa bweni utatakiwa kumpa nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo, godoro na vifaa vya malazi na usafi.

2.5 Mahitaji mengine ya kibinadamu kama vile ndoo moja ya lt.20, jembe 1 lenye mpini,fagio 1 ya chelewa na fagio ya kusukumia maji (mopa) na file ndogo 2.

3.0 **Sheria na kanuni muhimu za shule hii.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu.. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).

d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;

e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote ; na

i) Kutunza mali za umma

3.2 Makosa Yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

a) Wizi

b) Uasherati na ushoga

c) Ubakaji

d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadharika

e) Kupigana au kupiga

f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

g) Kudharau Bendera ya Taifa

h) kuwa mjamzito / kupata mimba

i) kuoa au kuolewa

j) Kotoa mimba

h) Kugoma , kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu

k) kukataa adhabu kwa makusudi

l) Kuwa na simu ya mkononi

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

a) Medical examination form ambayo ijazwe na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.

b) Fomu ya mzazi ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai

c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhari soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

……

ELIZABETH J. MALIGA

MKUU WA SHULE

OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI KIWELE

FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA KIDATO CHA …….....

(Sehemu ya kwanza ya fomu hii ijazwe na mwanafunzi na sehemu ya pili ijazwe na mzazi)

1. Mimi…… (Mwanafunzi). Kwa hiari yangu nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha kwanza (I) katika Shule ya Kiwele sekondari. Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. Naahidi kutomiliki simu kwa kipindi chote niwapo shuleni.

   Jina la mwanafunzi……

   Sahihi ya mwanafunzi …….

   Tarehe……
2. Sehemu hii ijazwe na mzazi/mlezi.

   Mimi…….....Mzazi/mlezi wa……

   …….naikubali/sikubali nafasi aliyopewa mtoto wangu na kwamba muda awapo shuleni atalazimika kuwa mtii kwa Walimu, wazazi, viongozi na jamii kwa ujumla. Atalazimika kufuata sheria zote za shule. Naahidi kuwa mwanangu atazifuata taratibu zote za shule hadi atakapomaliza shule.

   Jina la Mzazi/mlezi…….

   Sahihi……..

   Tarehe……..

OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI KIWELE

FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULE

HABARI ZA MZAZI/MLEZI

(Fomu hii ijazwe na mzazi/ mlezi)

1. Jina kamili la baba ……
2. Uraia ……
3. Kazi yake ……..
4. Jina kamili la mama ……..
5. Uraia …….
6. Kazi yake ……
7. Jina kamili la mlezi (iwapo haishi na wazazi wake)……
8. Mtoto anaishi na (1) Baba tu (2) Mama tu (3) Wazazi wote (4) mlezi (kata yasiyohusika).
9. Dini ya mzazi/mlezi ……
10. Dhehebu unalotaka mwanao alelewe …….
11. Anuani kamili ya sehemu ambako mtoto atakuwa anakwenda wakati wa likizo……
    ……
12. Mimi ……. Mzazi/mlezi wa …….. nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi. Naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri mchapa kazi, na mwenye bidii.

NB: HURUHUSIWI KUMPA MWANAO SIMU PINDI AJAPO SHULENI NA KWA MUDA WOTE AWAPO SHULENI.

…….. …….

Sahihi ya mzazi/mlezi. Tarehe

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY

KIWELE SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by medical officer in suspect of all new students)

Full name ……..

Age …….

1. Blood count (red and white) ……..
2. Urine examination …… ….
3. Stool examination ……...
4. Syphilis test …….
5. T.B test ……
6. Ear test ……..
7. Eye test …….
8. Spleen ……...
9. Abdomen ……..
10. Addition information or any other physical, mental, hereditary of infectious

    ……

    ……

    Treatment after examination.

    ……

    …….

<u>MEDICAL CERTIFICATE</u>.

I certificate that the above concerned has been examined and found fit into pursue for further education.

Signature …….

Designation …….

Station …….

(Official Stamp) ……..

Date …….

NB: Fomu hii ijazwe na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikalini.